

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO



Tarehe: 18.08.2022

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro imepokea kibali cha ajira mpya chenye **Kumb. Na. FA.170/371/01/145** cha tarehe **22 Juni, 2022**.

Kufuatia kibali tajwa hapo juu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro anawatangazia Watanzania wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro kutuma maombi ya kazi kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ndani ya siku **14** kuanzia tarehe ya Tangazo hili.

AFISA MTENDAJI WA KIJIKI III NAFASI (3)

SIFA ZA KUAJIRIWA.

- a) Awe Raia wa Tanzania na mwenye akili Timamu.
- b) Awe na umri usiopungua miaka **18** na usiozidi miaka **45**.
- c) Kuajiriwa mwenye Elimu ya kidato cha nne IV au sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/cheti (NTA Level 5) katika moja ya fani zifuatazo:

Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIKI

- i. Katibu wa kamati ya Kijiji.
- ii. Mtendaji Mkuu wa Kijiji.
- iii. Mratibu wa utekelezaji wa Sera na Sheria zinazotekelezwa na Halmashauri katika Kijiji.
- iv. Mshauri wa Kamati ya Kijiji kuhusu mipango ya Maendeleo katika Kijiji.
- v. Msimamizi wa Utekelezaji wa Sheria ndogo pamoja na sheria nyingine zinazotumika katika Kijiji.
- vi. Mshauri wa Kamati ya Kijiji kuhusu masuala ya Ulinzi na Usalama.
- vii. Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kutunza kumbukumbu za walipa kodi wote.
- viii. Kuandaa na kutunza rejesta ya wakazi wote na
- ix. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

MSHAHARA

Ngazi ya mshahara **TGS B**, sawa na **Tshs 450,000/=** kwa mwezi.

MAELEZO YA JUMLA

- a) Barua za maombi ziambatanishwe na nakala za vyeti vya Elimu/Taaluma na cheti cha kuzaliwa, CV.
- b) Waombaji wa nafasi hii wanalazimika kuwa na namba ya Utambulisho wa Uraia National (Identification Number) kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).
- c) Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimekaguliwa na kuthibitishwa na Mamlaka husika.
- d) Tustimonials, provisional results, Statement of Results na hati za matokeo ya kidato cha nne na sita (Form IV na form VI result slips) havitapokelewa

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe: **01/09/2022** saa **9:30** Alasiri

Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya Ngorongoro,
55 Barabara ya Mkapa,
23782 ORGOSOROK, NGORONGORO.

Tangazo limetolewa na;


Dkt. Jumaa Mohamed Mhina
**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
NGORONGORO.**

**MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO**



Jiandae kuhesabiwa siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022